Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

# HISTORIA YA LUGHA

1. Wakati wa ukoloni, Kiswahili kilienea zaidi Tanzania kuliko Kenya na Uganda. Taja sababu **tano (5)** zilizosababisha hali hiyo.
2. Eleza jinsi shughuli za Waarabu zilivyosaidia kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kabla ya uhuru.
3. Baada ya Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya taifa vyombo mbalimbali viliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili. Fafanua kuhusu uundwaji wa asasi tano (5) zilizoanzishwa kwa minajili hiyo.
4. Kwa kutumia mifano, thibitisha ubantu wa Kiswahili kwa hoja madhubuti nne (4).
5. Fafanua athari ya Waarabu katika lugha ya Kiswahili kwa kutoa hoja nne (4).
6. Kwa kutumia mifano, onesha jinsi shughuli za dini, utawala, biashara na elimu zinavyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.
7. Kwa kutumia hoja tano, onesha juhudi za Wajerumani katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini wakati wa utawala wao.
8. Kwa kutumia hoja tano, fafanua jinsi utawala wa Waingereza ulivyoimarisha Kiswahili nchini Tanzania kwa kupitia mfumo wa elimu.
9. Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) ni miongoni mwa taasisi zilizojitahidi katika kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika. Eleza majukumu matano ya chama hiki katika kufanikisha azma hiyo.
10. a) Andika lahaja tano za Kiswahili
    b) kabla ya uhuru, Waarabu walitumia njia gani ambazo zilisaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania?
11. a) Taja maana tano za mswahili.
    b) Eleza shughuli za utawala za Wajerumani kabla ya uhuru zilizosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili.
12. Kwa kutumia mifano mitatu (3) dhahiri fafanua mfanano wa tungo za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.
13. Taasisi ya Elimu (TET) na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ni miongoni mwa asasi zilizoanza mara tu baada ya uhuru. Fafanua kazi tatu kwa kila moja katika kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania.
14. “Sifa ya lugha ni kuwa na uwezo wa kupokea msamiati kutoka lugha za kigeni.” Kwa kutumia mifano, eleza sababu nne zilizokifanya Kiswahili kuwa nameno mengi ya Kiarabu kuliko kutoka lugha nyingine za kigeni.
15. Kwa kutumia mifano na kutoa hoja mbili kwa kila moja, eleza kwa ufupi mafanikio ya lugha ya Kiswahli enzi za Waarabu katika:
    (i) Dini
    (ii) Biashara
16. Kwa kutumia hoja tano zenye mifano, eleza kwa kifupi mchango wa wamisionari wa kikristo katika kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru.
17. Kwa kutumia hoja nne, eleza jinsi misafara ya biashara ilivyofanikisha kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania kabla ya uhuru.
18. Kwa kutumia hoja nne na mifano, fafanua mchango wa vipindi mbalimbali vya redio katika kuimarisha lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

MASWALI YA SARUFI

1. Tunga tungo yenye vipashio vifuatavyo
   (a) Nomino + Kishazi tegemezi + Prediketa + Shamirisho.
   (b) Kiima kapa + Prediketa + Chagizo.
   (c) Kirai nomino + Kishazi huru + Kishazi tegemezi.

2. Eleza dhima ya kiambishi "ni" kilichopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
   (a) Alini saidia.
   (b) Wajumbe wapo mkutanoni .
   (c) Wakubalieni .
   (d) Yeye ni mvivu.
   (e) Nina kalamu.

3 Bainisha kauli **tano (5)** za vitenzi na kila kauli itungie sentensi moja.

4 Kwa kutumia mifano ya sentensi eleza dhima **tano (5)** za mofimu "ku".

5. Viambishi awali na viambishi tamati vina uwezo wa kubadili umbo na maana ya neno. Katika maneno yafuatayo eleza dhima ya kila kiambishi.
   (a) Watakapotupambanisha.
   (b) Sielekezi.
4. Upatanisho wa kisarufi hufanya nomino mbalimbali kuwa katika kundi moja. Fikiria nomino tano na kwa kutumia sentensi moja kwa kila nomino zipange katika makundi yake.
5. Uchanganuzi wa sentensi hufanyika hatua kwa hatua. Ukitumia hatua hizo changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali.
   Wale wawili watakuwa wamepimwa virusi vya UKIMWI hivyo afya zao zitakuwa nzuri.
6. Eleza njia zilizotumika kuunda misamiati ifuatayo katika lugha ya Kiswahili.
   (a) Sigara.
   (b) Mwanajeshi.
   (c) Kipima pembe.
   (d) Pembe tatu.
   (e) Mtutu.
7. "Vitenzi vifuatavyo vinatofautiana kiasili". Toa sababu za kuthibitisha jibu lako, kisha vipange vitenzi hivyo kutegemeana na uasili wake.
   (a) Lima (b) Arifu (c) Ruka (d) Sali (e) Pamoja
   (f) Adhibu (g) Weka (h) Buni (i) Stahimili (j) Chambua.
3. Vitenzi vya Kiswahili vina tabia zake. Kwa kutumia mifano ya sentensi tano (5) onesha tabia tano tofauti za vitenzi.
4. Kuna tofauti gani kati ya mofimu huru na mofimu tegemezi? Eleza kwa kutumia sentensi nne (4), mbili (2) kwa kila mofimu.
5. (a) Eleza maana ya vidahizo vifuatavyo:
   (i) Kinyenyezi
   (ii) Matandu
   (iii) Matlaba
   (iv) Sandali
   (v) Uzimbezimbe
   (b) Tunga sentensi moja (1) kwa kila kidahizo.
6. Vitenzi vishirikishi hukamilisha ujumbe katika sentensi. Kwa kutumia mifano mitano (5) thibitisha ukweli huo.
7. Fafanua dhana ya kiunganishi huru. Kwa kutumia mifano dhihirisha tofauti kati ya kiunganishi huru na aina nyingine ya kiunganishi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

8. Eleza tofauti za msingi mbili (2) zilizopo kati ya kirai na kishazi. Toa mifano miwili kwa kila tofauti.
9. Ni kigezo kipi kinachotumika katika kuunda ngeli za kimapokeo? Dhihirisha utumiaji wa kigezo hicho kwa kutunga sentensi tano (5) za ngeli tofauti.
10. Kwa kutoa mifano, taja matumizi matano (5) tofauti ya kiunganishi "Kwa".
11. Eleza tofauti kati ya viambishi awali na viambishi tamati. Toa maoni yako kuhusu dhana ya viambishi "kati" katika Kiswahili.
12. "Mofimu huru zina hadhi ya neno." Fafanua usemi huu kwa kutumia sentensi tano (5) tofauti.

13. Tumia kiambishi "KA" kuonesha matukio kumi (10).
14. "Kila lugha ina tabia ya kuchukua maneno kutoka lugha nyingine ili kukidhi mahitaji yake kimsamiati." Fafanua kauli hii ukitumia maneno kumi (10) ya Kiswahili.
15. Yapange maneno yafuatayo kama yanavyoonekana katika kamusi, kisha eleza maana ya kila neno kwa kutoa mfano mmoja (1) wa sentensi.
    (a) Falsafa (b) Barizi (c) Anuwai(d) Barubaru
    (e) Kinda (f) Ajuza (g) Fanusi (h) Ghaibu
    (i) Goigoi (j) Kinanda
16. Eleza maana ya upatanisho wa kisarufi. Fafanua jibu lako kwa kutoa mifano minne.
17. Kwa kutumia mifano dhahiri, fafanua dhana zifuatazo:
    (a) Kiima
    (b) Chagizo
    (c) Shamirisho
    (d) Utohoaji
    (e) Urudufishaji
18. "Maneno huweza kubadilika kutoka aina moja na kuwa aina nyingine." Dhihirisha kauli hii kwa kubadili maneno yafuatayo kwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika mabano.
    (a) Mkono (badili kuwa kielezi) (f) Bisha (badili kuwa kivumishi)
    (b) Kwenda (badili kuwa nomino) (g) Refu (badili kuwa kitenzi)
    (c) Bora (badili kuwa kitenzi) (h) Linda (badili kuwa nomino)
    (d) Ogopa (badili kuwa kivumishi) (i) Kabati (badili kuwa kielezi)
    (e) Mzazi (badili kuwa kitenzi) (j) Uguza (badili kuwa nomino)
19. Kamusi ni muhimu kwa mtumiaji yeyote wa lugha. Taja hoja tano zinazothibitisha umuhimu huo.
20. Kwa kutumia mifano ya lugha ya Kiswahili, taja sababu tano za utata katika mawasiliano.
21. Kwa kutumia mifano, taja miundo mitano ya kirai nomino.

22. Onesha nomino katika tungo zifuatazo kisha bainisha ni aina gani ya nomino:
    (a) Hatuna budi kumshukuru Mola.
    (b) Mazao yamestawi shambani.
    (c) Uzalendo usisitizwe shuleni.
    (d) Mpeleke mtoto ndani.
    (e) Nimechoshwa na upweke.
23. Andika tungo zifuatazo kwa usahihi:
    (a) Mwenyekiti alihairisha kikao.
    (b) Mtoto amedumbukia shimoni.
    (c) Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia deksi.
    (d) Mama amenunua dazani ya sufuria.
    (e) Mwanafunzi msafi amepewa zawadi.
24. Tambulisha viambishi vyenye dhima zilizowekwa kwenye mabano katika maneno yafuatayo:
    (a) Hakukumbuka (njeo ya wakati uliopita)
    (b) Wamekamatana (kauli ya kutendana)
    (c) Akisema (hali ya masharti)

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(d) Ananiona (kurejesha mtendwa)
(e) Tuliwashangilia (kurejesha watenda)
(f) Huimba (hali ya mazoea)
(g) Wamelima (wakati uliopita hali timilifu)
(h) Wanatucheka (urejeshi wa watendwa)
(i) Hawakusoma (ukanushi)
(j) Amenipigisha (kauli ya kutendesha)

25. Onesha maana tano za neno "kata" na kwa kila maana tunga sentensi moja.
26. "Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimojawapo kati ya vigezo vya kuunda ngeli za nomino." Thibitisha dai hilo kwa kutunga sentensi ukitumia ngeli zifuatazo:
    (a) U-I
    (b) LI-YA
    (c) U-ZI
    (d) I-ZI
    (e) U-YA

27. Fafanua utata uliopo katika sentensi zifuatazo:
    (a) Mama anafurahia pango.
    (b) Mwalimu analima barabara.
    (c) Alimpigia ngoma.
    (d) Kijana amepata fomu.
    (e) Baba anaunda.
28. Tumia neno "Paa" katika sentensi kuunda dhana zifuatazo:
    (a) Nomino
    (b) Kitenzi
    (c) Kielezi
    (d) Kivumishi
    (e) Shamirisho

29. Bainisha mzizi wa asili kwa kila neno katika maneno yafuatayo:
    (a) Anawaandikisha
    (b) Mkimbizi
    (c) Mlaji
    (d) Muumbaji
    (e) Nisingelipenda
    (f) Kuburudika
    (g) Sadifu
    (h) Aliokota
    (i) Walichopoka
    (j) Kipambanuliwe
30. Vibadilishe vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya kutendeka:
    (a) Badili
    (b) Kata
    (c) Komboa
    (d) Zuia
    (e) Fika
    (f) Zoa
    (g) Jenga
    (h) Remba
    (i) Tumia

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(j) Lima

31. Fafanua maana ya neno “chenga” kwa kutumia sentensi tano tofauti.

Watumiaji wa lugha ya Kiswahili hufanya makosa mengi bila ya kudhamiria. Taja aina mbili za makosa hayo kwa kutoa mfano wa sentensi mbili kwa kila kosa.

32. . (a) Eleza maana ya rejesta.
(b) Kwa kutoa mifano, taja mambo muhimu matatu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta.

33. Katika kila sentensi andika neno moja lenye maana sawa na maelezo ya sentensi husika.
(a) Mtu anayechunguza uhalifu.
(b) Ng’ombe dume aliyehasiwa.
(c) Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma.
(d) Mti unaozaa matunda yanayotengenezwa kinywaji cha kahawa.
(e) Sehemu ndogo ya nchi iliyochongoka na kuzungukwa na bahari katika sehemu zake tatu.

34. Eleza dhima za mofimu "li" kama ilivyotumika katika sentensi zifuatazo:
(a) Shamba letu li kubwa sana.
(b) Walishelewa kurudi.
(c) Tunalifuatilia.
(d) Limeharibika.
(e) Shikilia.

35. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya ukanushi:
(a) Ameshiba sana.
(b) Watoto wengi wanaogelea.
(c) Mvua ilinyesha kwa wingi sana.
(d) Kijana anakula chakula kingi.
(a) Eleza maana ya utohoaji.
(b) Maneno yafuatayo yametoholewa kutoka lugha gani?
(i) Picha (ii) Duka (iii) Shule
(iv) Rehema (v) Shati (vi) Trekta
(vii) Ikulu (viii) Bunge (ix) Achali

36. Taja aina za sentensi zifuatazo kisha eleza muundo ujengao kila sentensi.
(a) Maisha ni safari ndefu.
(b) Ukisoma kwa bidii utafaulu kwa kiwango cha juu.
(c) Mtoto aliyelazwa hospitalini ameruhusiwa kwenda nyumbani.
(d) Nitakuja leo ingawa nitachelewa sana.
(e) Alinunua madaftari lakini kitabu cha Kiswahili alipewa na mwalimu.

37. (a) Eleza maana ya urejeshi katika kitenzi.
(b) Tunga sentensi tatu zinazoonesha urejeshi wa:
(i) Mtenda nafsi ya tatu umoja.
(ii) Mtendwa (idadi - wingi).
(iii) Mtenda (kitu).

38. Andika maneno matano ambayo yameundwa kutokana na kufananisha sauti. Kwa kila neno tunga sentensi moja.

39. (a) Eleza maana ya Kiambishi.
(b) Bainisha viambishi vilivyopo katika vitenzi vifuatavyo:
(i) Tunalima.
(ii) Wanatembea.
(iii) Godoro.
(e) Mimi nasoma polepole.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

37. Fafanua dhana zifuatazo na kisha toa mfano mmoja kwa kila dhana uliyofafanua.
    (a) Neno
    (b) Kirai
    (c) Kishazi
    (d) Sentensi
    (e) Kamusi

38. Nyambua maneno yafuatayo ili kupata maneno mawili zaidi kwa kila neno;
    (a) beba
    (b) pokea
    (c) rudi
    (d) soma
    (e) shughuli
    (f) sema
    (g) penda
    (h) heshima
    (i) pigo
    (j) pika

39. Bainisha tabia za maumbo yaliyokolezwa wino katika vitenzi ulivyopewa.
    (a) **Futa** ubao.
    (b) **Hu**tafaulu mtihani.
    (c) Ame **tu**alika.
    (d) Mtoto **hu**lia mara nyingi.
    (e) Yeye **ni** mwalimu.
    (f) Mgonjwa ame **ji**laza chini.
    (g) Wana **vi** oma **vi**tabu vyao.
    (h) Paka amepi**gwa** .
    (i) Mti umekat**ika** .

40. (a) Eleza maana na dhima ya kiunganishi katika sentensi.
    (b) Tunga sentensi mbili kwa kila kiunganishi kifuatacho;
    (i) kwa sababu
    (ii) kwamba
    (iii) ingawa
    (iv) lakini

41. "Kuambatanisha maneno ni namna mojawapo ya kuzalisha maneno mapya katika lugha ya Kiswahili." Bainisha njia tatu za kuambatanisha maneno kisha toa mifano miwili kwa kila njia uliyobainisha.

42. Taja njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:
    (a) Amirijeshi
    (b) Kiswahli
    (c) Kifaru
    (d) Chajio

43. Andika nahau yenye maana sawa na tungo zifuatazo:
    (a) Jumanne ni kijana mchoyo.
    (b) Yule ni mropokaji sana.
    (c) Malingumu ni mwizi.
    (d) Mwalimu wetu ameoa.

44. (a) Kwa kutumia njia ya mnyumbuliko, unda nomino mbili kwa kila kitenzi kifuatacho:
    (i) Piga

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(ii) Lima
(iii) Pika
(iv) Cheza

(b) Tunga tungo moja kwa kila kipengele (i) - (iv) ukizingatia viambajengo vya kila moja:
(i) Kishazi tegemezi + Kishazi huru
(ii) Kishazi huru
(iii) Kishazi tegemezi
(iv) Kishazi huru + Kishazi huru

45. (a) Soma kwa makini sentensi (i) hadi (iv), kisha fafanua kwa pamoja vipengele vinne vinavyodhihirisha uhusiano baina ya Kiswahili na lugha za Kibantu.
(i) Mtoto amelala (Kiswahili)
(ii) Mwana agonili (Kingoni)
(iii) Mwana yagonile (Kigogo)
(iv) Omwana yanagila (Kihaya)

46. Kwa kutumia mifano, eleza chanzo cha misimu na toa dhima tano za misimu.

45. Kwa kila tungo zifuatazo onesha kivumishi kisha taja aina ya kivumishi hicho

a) Kikombe cha kaka kimevunjika
b) Wachezaji wetu wanatafuta mpira
c) Mchana mrembo anajikwatua
d) Viatu vyote vimechafuka
e) Wanafunzi wachache wamenunua vitabu.

48. Lugha inapotumika vibaya huweza kupotosha lengo la msemaji. Fafanua ukweli wa usemi huu kwa mifano mitano.

49. Fafanua dhima ya ‘ji’ katika maneno yafuatayo

a) Jitu
b) Uzalishaji
c) Unajikwatua
d) Jicho

50. kwa kutumia mifano eleza maana ya

a) Kamusi wahidiya
b) Rejesta
c) Misemo
d) Lahaja
e) Lugha ya mazungumzo

46 Eleza maana ya utohoaji.
(b) Maneno yafuatayo yametoholewa kutoka lugha gani?
(i) Picha (ii) Duka (iii) Shule
(iv) Rehema (v) Shati (vi) Trekta
(vii) Ikulu (viii) Bunge (ix) Achali

47. Taja aina za sentensi zifuatazo kisha eleza muundo ujengao kila sentensi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(a) Maisha ni safari ndefu.
(b) Ukisoma kwa bidii utafaulu kwa kiwango cha juu.
(c) Mtoto aliyelazwa hospitalini ameruhusiwa kwenda nyumbani.
(d) Nitakuja leo ingawa nitachelewa sana.
(e) Alinunua madaftari lakini kitabu cha Kiswahili alipewa na mwalimu.

48. (a) Eleza maana ya urejeshi katika kitenzi.
(b) Tunga sentensi tatu zinazoonesha urejeshi wa:
(i) Mtenda nafsi ya tatu umoja.
(ii) Mtendwa (idadi - wingi).
(iii) Mtenda (kitu).

49. Andika maneno matano ambayo yameundwa kutokana na kufananisha sauti. Kwa kila neno tunga sentensi moja.

50. (a) Eleza maana ya Kiambishi.
(b) Bainisha viambishi vilivyopo katika vitenzi vifuatavyo:
(i) Tunalima.
(ii) Wanatembea..
(iii) Godoro.

Taja njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:
(a) Amirijeshi
(b) Kiswahli
(c) Kifaru
(d) Chajio

51. Andika nahau yenye maana sawa na tungo zifuatazo:
(a) Jumanne ni kijana mchoyo.
(b) Yule ni mropokaji sana.
(c) Malingumu ni mwizi.
(d) Mwalimu wetu ameoa.

52. (a) Kwa kutumia njia ya mnyumbuliko, unda nomino mbili kwa kila kitenzi kifuatacho:
(i) Piga
(ii) Lima
(iii) Pika
(iv) Cheza
(b) Tunga tungo moja kwa kila kipengele (i) - (iv) ukizingatia viambajengo vya kila moja:
(i) Kishazi tegemezi + Kishazi huru
(ii) Kishazi huru
(iii) Kishazi tegemezi
(iv) Kishazi huru + Kishazi huru

Kwa kuzingatia tungo ulizopewa, bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari:
(a) Juzi tulishiriki maandamano ya amani.
(b) Kucheza kwake kunaburudisha.
(c) Kijana mlevi amepata ajali.
(d) Hamisi alikuwa amekwisha kwenda kulima .
(e) Wale vikongwe wamepata msaada.
(f) Mawazo hayo si yangu.
(g) Sitakwenda kwake asilani!
(h) Amekwenda kazini ijapokuwa ni mgonjwa.
(i) Hiki kitawekwa ukumbini.
(j) Mbuzi amekwisha kata kamba.

53. Unganisha tungo zifuatazo kwa kutumia O-rejeshi:
(a) Mafisadi wamekamatwa. Mafisadi wamefikishwa mahakamani.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(b) Kitabu kimenunuliwa. Kitabu kipo kabatini.
(c) Mfadhili amepatikana. Mfadhili mkarimu sana.
(d) Hukumu imetolewa. Hukumu ni ya haki.
(e) Mahali pameandaliwa. Mahali hapatoshi.

54. Bainisha kauli zinazowakilishwa na vitenzi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo:
(a) Refa alichezesha mechi vizuri.
(b) Mtoto amevunjwa mguu.
(c) Wanafunzi wanasomeana kitabu.
(d) Mafuta yamemwagika.
(e) Walevi wanapigana kilabuni.
(f) Mtoto analia sana.
(g) Babu alisomewa kitabu.
(h) Dada anampikia mtoto uji.
(i) Kaka alimtuliza rafiki yake.
(j) Gazeti linasomeka vizuri.

55. Vishazi tegemezi hufanya kazi ya vivumishi viwapo katika tungo. Onesha ukweli wa kauli hiyo kwa kutumia mifano minne ya sentensi.

56. Toa maana ya kamusi kisha fafanua sehemu kuu tatu zinazounda kamusi.

Sentensi zifuatazo zina makosa. Onesha kosa kisha andika upya sentensi hizo kwa usahihi.
(a) Nimekwenda kwa Kondo na nimemkuta hayupo.
(b) Dhumuni la Ali ni kuishi mjini.
(c) Tunachukua nafasi hii kuwakaribisha hapa nyumbani.
(d) Mahusiano mazuri hujenga undugu.
(e) Ni muhimu tukaelewa taratibu za lugha yetu.

57. Kuna njia nyingi za kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili. Eleza njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:
(a) Msikwao
(b) Jografia
(c) Chemshabongo
(d) Mchezaji
(e) Kisimbuzi.

58. Tumia maneno yaliyowekwa kwenye parandesi kuunganisha sentensi zifuatazo:
( **kwa; licha ya; pasi na; pamoja na; kwa sababu** )
(a) Kijana huyu anaingia chumbani. Kijana anaingia bila hodi.
(b) Juma hakusalimia wazee. Juma hakuwaona wazee.
(c) Rashidi ni mrefu. Mimi ninamshinda kwa mbio.
(d) Wewe ni mwanafunzi lakini lazima ulipe nauli.
(e) Mchezaji amerusha mpira. Mchezaji amefuata utaratibu.

59. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya utumizi wa lugha.
(b) Taja mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuteua lugha ya kutumia, kisha toa mifano miwili kwa kila moja.

60. Fafanua maana ya neno " **bichi** " kama lilivyotumika katika tungo zifuatazo kwa kuzingatia muktadha husika:
(a) Niletee shuka la kijani **kibichi.**
(b) Hili embe bado ni **bichi.**
(c) Msichana huyu ni **mbichi** kabisa.
(d) Chakula hiki ni **kibichi** .
(e) Koti lake ni **bichi**

61. Soma sentensi zifuatazo kisha kwa kila moja taja ni aina gani ya sentensi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(a) Mtoto alikuwa anakimbizana na wenzake.
(b) Akisema ukweli atasamehewa.
(c) Wanafunzi wanasoma kitabu na mwalimu anaandika ubaoni.
(d) Kitabu kilichonunuliwa jana kitaletwa kesho darasani.
(e) Ingelikuwa vyema tungelifahamiana leo.

62. Taja njia iliyotumika kuunda maneno yafuatayo:
(a) Megawati
(b) Tunasherehekea
(c) Kifudifudi
(d) Kasimawimbi
(e) Nyau
(f) Uzalishaji
(g) Pekepeke
(h) Pedeli
(i) Ufagio
(j) Kingamwili

63. Badilisha nomino zifuatazo ili ziwe vitenzi vilivyo katika kauli ya kutenda:
(a) Hakimu
(b) Msamaha
(c) Msuluhishi
(d) Kinyambuo
(e) Uhamiaji
(f) Mafichioni
(g) Shuhuda
(h) Masimulizi
(i) Vichekesho
(j) Upendo.

64. Tungo zifuatazo ni tata, toa maana mbili kwa kila tungo:
(a) Wewe una ua?
(b) Watoto wanamkimbilia Babu.
(c) Kaka amenunua taa.
(d) Kumbe ni tembo?
(e) Sawa, sasa unaweza kuandaa sherehe.

65. Eleza maana ya vidahizo vifuatavyo kisha tunga sentensi moja kwa kila kidahizo.
(a) Lambo
(b) Sherasi
(c) Makala
(d) Pogoa
(e) Umbeja

MASWALI YA UANDISHI

1. Muundo wa uandishi wa barua za kirafiki na barua za kikazi ni tofauti. Thibitisha kauli

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

hiyo.

2. Manyanda akiwa mfanyakazi wa kiwanda cha korosho Tanita alipewa taarifa kuhusu ugonjwa wa baba yake. Wewe kama Manyanda andika barua ya kuomba ruhusa. Anuani ya kiwanda ni S.L.P. 1030, Kibaha.

3. Andika insha yenye maneno mia **moja (100)** kuhusu moja ya mada zifuatazo:
   (a) Maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2005.
   (b) Upimaji wa virusi vya Ukimwi.
   (c) Mwenda tezi na omo marejeo ngamani.

4. Andika insha yenye maneno 250 kuhusu moja ya mada zifuatzo:
   (a) Aisifuye mvua imemnyeshea.
   (b) Elimu ya msingi ina umuhimu wake katika jamii.
   (c) Maradhi yanavyorudisha nyuma maendeleo ya familia hatimaye Taifa.
   (d) Kuelimika kwa msichana ni kuelimika kwa jamii.
   (e) Wanyama pori.

5. Katika kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwako, unahitaji marafiki kwa ajili ya kusherehekea siku hiyo. Andaa kadi ya mwaliko ili kuwapa taarifa rafiki zako.
6. Eleza tofauti iliyopo kati ya hotuba na risala. Andika hotuba kuhusu “Maji ni Uhai.”
7. Wewe kama afisa ununuzi, andika barua kwa mfanyabiashara mashuhuri wilayani kwenu kuhusu agizo la bidhaa.
8. Andika insha isiyo ya kisanaa yenye maneno mia mbili na hamsini (250) kuhusu mandhari ya shule yenu.
9. Andika kumbukumbu za kikao cha wanafunzi kuhusu sherehe ya kumuaga mkuu wenu wa shule aliyepata wadhifa wa kuwa Afisa Elimu wa Mkoa.
10. Jifanye kuwa umepata barua ya mwaliko wa sherehe ya siku ya kuzaliwa kwa rafiki yako aitwaye Faraja Matata, itakayofanyika siku ya tarehe 10/10/2012. Kwa bahati mbaya siku tatu kabla ya sherehe umepata safari ya kikazi kuelekea mkoani Singida. Andika barua kumtaarifu rafiki yako kuwa hutaweza kuhudhuria sherehe hiyo. Jina lako liwe Tumaini Baraka.
11. Andika insha yenye maneno yasiyopungua mia mbili na hamsini (250) na yasiyozidi mia tatu (300) kuhusu umuhimu wa huduma za simu ya mkononi.
12. Wewe ni mfanyabiashara mashuhuri mjini Dodoma. Andika barua ya kutuma bidhaa kwa mteja wako aitwaye Dunia Msimbo anayeishi Lindi. Jina lako liwe Nyila Sasisha.
13. Andika tangazo kwenye gazeti la Rai ukitoa taarifa kuhusu kupotea kwa mwanao aitwaye Raha Karaha, jina lako liwe Furaha Machupa.
14. Andika insha yenye maneno yasiopungua mia mbili (200) na yasiozidi mia tatu (300) kuhusu methali isemayo “Samaki Mkunje angali mbichi”.
15. Wewe ni mwenyekiti wa mtaa ambao umekumbwa na mafuriko lakini wananchi wako wanakataa kuhamia makazi mapya. Andaa hotuba utakayoitoa kwa wananchi wa mtaa wako ili uwashawishi kuondoka katika sehemu hiyo. Jina la mtaa ni Kwamachombo na eneo la makazi mapya linaitwa Kitivo.
16. Jifanye wewe ni Gudhah Mukish anayeishi mtaa wa Tandamti - Gerezani Kariakoo na unataka kuuza gari yako aina ya TOTYOTA CARINA. Andika tangazo kwenye gazeti la Mwananchi.
17. Andaa kadi ya mwaliko kwa rafiki zako ili washiriki katika mahafali ya kumaliza Kidato cha Nne yatakayofanyika shuleni kwako siku ya Jumamosi tarehe 21/11/2015, kisha kufuatiwa na tafrija fupi itakayoandaliwa na wazazi wako katika ukumbi wa Kijiji mnamo saa 10.00 jioni. Jina lako liwe SiliSilali wa SHule ya Sekondari Kiriche.
18. Andika mambo matano ya kuzingatia katika utungaji wa insha. Fafanua umuhimu wa kila jambo.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

19. Andika risala kwa niaba ya wanafunzi wenzako mnaohitimu kidato cha nne katika shule ya sekondari Kwedukwazu. Mgeni rasmi ni Afisa elimu wa mkoa.
20. Kwa niaba ya shirika la umeme la Tanzania, andika tangazo katika gazeti la mwananchi ukiwajulisha wananchi wa Yombo Dovya kuhusu tatizo la kukatika umeme siku ya tarehe 4/ 11/2020. Jina lako liwe Jimbi Tambitambi.
21. Andika insha isiyozidi maneno mia tatu (300) na isiyopungua mia mbili na hamsini (250) kuhusu faida za televisheni kwa jamii.
22. Umechaguliwa kutoa risala kwa niaba ya wanakijiji wa kijiji cha Kisombogho, wanaotaka kutoa shukrani zao kwa Mkuu wa Wilaya aliyewachimbia kisima cha maji kijijini hapo. Andika risala utakayoisoma siku ya kikao.
23. Tofautisha muundo wa barua rasmi na barua za kindugu/kirafiki.
24. Jifanye kuwa mfanyabiashara wa mchele na unataka kuitangaza biashara yako nje na ndani ya nchi. Andika tangazo kuhusu biashara hiyo na jina lako liwe Pera Mlavi.
25. Wewe ni mshiriki wa shindano la uandishi wa insha lililoandaliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa. Kaulimbiu ya shindano ni "Watoto zingatieni daima maonyo ya wazazi wenu". Kwa kutumia kauli mbiu hii, andika insha ya kisanaa isiyopungua maneno mia mbili (200) na isiyozidi maneno mia mbili hamsini (250), yenye kuishia na methali "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu".
26. Wewe ni Kiranja Mkuu wa Shule ya Sekondari Kazamoyo iliyoko Tanga, jina lako Uwezo Jitihada na unasoma kidato cha nne. Andika barua kwa Mkuu wa Shule ukiomba ruhusa ya kuhudhuria semina ya uelimishaji rika takayofanyika tarehe 10/11/2013 katika Shule ya Sekondari Tutafika iliyoko Moshi. Barua yako ipitie kwa Mwalimu wa Darasa.
27. Jifanye wewe una elimu ya kidato cha nne, jina lako Situmai Kasheshe unayeishi kijiji cha Songambele kilichopo wilayani Mpanda. Tumia taarifa zilizomo kwenye tangazo lifuatalo lililotolewa kwenye gazeti la Mwananchi la tarehe 01/12/2013 kuandika barua ya maombi ya kazi.

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**
**Kazi** : Karani Masijala
**Sifa** :

- Awe amehitimu kidato cha nne na kufaulu masomo ya Kiingereza na Hisabati
- Awe na umri usiozidi miaka 35
- Awe Mtanzania
- Awe na ujuzi wa kompyuta

Barua ya maombi iambatanishwe na nakala za vyeti na itufikie kabla ya tarehe 15/12/2013.
Maombi yote yatumwe kwa:
Afisa Mwajiri
Kampuni ya Kutengeneza Masufuria
S.L.P 600
KATAVI.

28. Andika insha isiyopungua maneno mia mbili hamsini (250) na isiyozidi maneno mia tatu (300) kuhusu "Madhara ya Operesheni Kimbunga."
29. Andika mambo ya kuzingatia katika kuandika kumbukumbu za mkutano wa mara ya pili.
30. Tumia kichwa cha habari "Faida nne za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za biashara nchini Tanzania" kuandika insha yenye maneno yasiyopungua mia tatu (300) na yasiyozidi mia nne (400).
31. Jifanye wewe ni diwani wa kata ya Kanyagatwende. Andika hotuba yenye maneno yasiyopungua mia tatu (300) na yasiyozidi mia nne (400) utakayoitoa kwa wananchi wako ukikemea tabia ya kuwachoma moto watu wanaosadikiwa kuwa ni wezi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Yameandaliwa na Madam Filieda Sanga 0753738704

Search ⇢ www.africona.net